

**Ripoti ya Kuhitimisha Mchakato wa Utatuzi wa Mzozo
Kuhusu Malalamishi Yaliopokelewa Kuhusiana na Uwekezaji wa IFC kwenye
Kampuni za Delonex Energy na Africa Oil (#33557 na #36699) nchini Kenya**

Mwezi wz tatu 2023

MHUTASARI

Ripoti hii ya kuhitimisha mchakato inaelezea kuhusu tathmini na mchakato wa utatuzi wa mzozo kuhusiana na malalamishi kuhusu mradi wa IFC wa mafuta na gesi nchini Kenya, na kuonyesha mambo ya kutafakari kuhusu na mafunzo yaliyopatikana kutokana na mchakato.

Mwezi wa Agosti mwaka wa 2019, CAO ilipokea malalamishi kutoka kwa shirika ya uraia linalopatikana nchini Kenya linalojulikana kama Kerio Valley Community Organization (KVCO) kwa niaba ya wanajamii 140 wanaoishi katika kaunti za Baringo, Elgeyo Marakwet, na Pokot Magharibi katika eneo la Kerio Valley nchini Kenya (“walalamishi”). Mbali na KVCO, walalamishi walisaidiwa na shirika linaloshughulikia masuala ya kisheria linalopatikana nchini Canada linalojulikana kama Justice and Corporate Accountability Project (JCAP). Malalamishi yalihusu athari kwa mazingira na kwa jamii kutokana na shughuli za utafiti wa kijiolojia za kutafuta mafuta na gesi zilizofanyika kwenye maeneo maalum katika Block 12A.¹ Wakati malalamishi yalipotolewa, IFC ilikuwa na miradi miwili inayohusiana na Block 12A: mojawapo na kampuni ya Delonex Kenya (One) Limited (Delonex) na mwingine na kampuni ya Africa Oil Corp (AOC).

CAO ilibaini kuwa malalamishi hayo yalikitidhi vigezo vya kuweza kutathminiwa mwezi wa Septemba mwaka wa 2019.² Wakati wa tathmini, Delonex na walalamishi (wahasika) waliamua kushughulikia masuala yaliyoibuliwa kupitia kitengo cha CAO cha Kutatua Mizozo. AOC walisema kuwa hawatashiriki kwenye mchakato huu kwa sababu walikuwa wamejiondoa kwenye Block 12A kabla ya malalamishi kutolewa kwa CAO na wala hawakuwahi kuendesha shughuli katika eneo hilo. Kutokana na pendekezo kutoka kwa wahasika, CAO iliweza kuwasiliana na mwendeshaji shughuli wa zamani kwenye eneo hilo, Tullow Kenya B.V. (Tullow), kampuni ambayo haikufadhiliwa IFC kuendesha mradi huu. CAO ilipowasiliana na Tullow, walikubali kushiriki katika mazungumzo yalilioendesha na CAO, hasa kama mwangalizi, iwapo wahasika wangeweza kukubaliana kuhusu usiri na kanuni za kuongoza kikao. Mwezi wa Oktoba mwaka wa 2020, mchakato wa tathmini ulikamilishwa, na kesi kuhamishiwa kwa awamu ya utatuzi wa mizozo wa CAO.

Walalamishi Delonex na Tullow (kama mwangalizi) walishiriki katika vikao vya kuwajengea uwezo na mikutano isiyokuwa ya pamoja kati ya Novemba mwaka wa 2020 na April mwaka wa 2021, na katika kikao cha kwanza cha pamoja kilichoongozwa na CAO mwezi wa Mei

¹ Block 12A ni eneo la zaidi ya kilomita 15,000 mraba na linalojumuisha kaunti za Baringo, Elgeyo Marakwet, Pokot Magharibi, Turkana, na Samburu katika eneo la Bonde la Ufa nchini Kenya.

² Vigezo vya CAO vya malalamishi kukubalika vinapatikana: <https://www.cao-ombudsman.org/how-we-work/intake-assessment>.

mwaka wa 2021. Tullow ilijiondoa kwenye mchakato mwezi wa Novemba mwaka wa 2021. Mchakato uliendelea baina ya walalamishi na Delonex hadi Agosti mwaka wa 2022, sanasana kupitia mikutano ya kandokando na wahusika.

Mwezi wa Agosti mwaka wa 2022, walalamishi walitoa wito kwa CAO kukomesha mchakato wa utatuzi wa mzozo na kuhamishia kesi hiyo kwa Kitengo cha Ridhaa cha CAO. Malalamishi haya yanahamishiwa kwa Kitengo cha Ridhaa cha CAO ili kutathminiwa, kwa kuzingatia Sera ya CAO.³

USULI

Miradi

Wakati malalamishi yalipotolewa katika mwaka wa 2019, IFC ilikuwa na miradi miwili iliyokuwa inaendelea inayohusiana na Block 12A: mojawapo na Delonex (iliyokuwa inaendesha shughuli kwa Block 12A kuanzia mwaka wa 2015 hadi mwaka wa 2021); na mradi mwingine na AOC (iliyokuwa inaendesha shughuli kwa Block 12A kuanzia mwaka wa 2010 hadi mwaka wa 2017). Kwa mjibu wa ufichuzi wa IFC, IFC ilifanya uwekezaji wa hisa zisizo na riba ya kudumu za thamani ya dola milioni 60 kwenye kampuni ya Delonex katika mwaka wa 2013 ili kuwezesha kununua vifaa, kufanya utafiti wa kijiolojia na ukuzaji wa rasilimali za Delonex katika maeneo ya Afrika Mashiriki na Afrika ya Kati kama sehemu ya orodha ya fedha zake zilizowekwa kwa faida, zilizolenga fursa za utafiti wa kijiolojia za kutafuta mafuta na gesi. Katika mwaka wa 2015, IFC ilifanya uwekezaji wa hisa zisizo na riba ya kudumu za dola za Marekani milioni 50 katika kampuni ya AOC na lengo kuu la kuwezesha utafiti wa kijiolojia wa kutafuta mafuta na gesi katika maeneo mbalimbali ya Lokichar Kusini (Block 10BB na Block 13T), na kutoa pia mtaji wa jumla uliohitajika kuendeleza shughuli za AOC.⁴ IFC iliainisha miradi yote miwili kuwa na uwezekano mkubwa wa kuwa na madhara mabaya kwa mazingira na/au kwa jamii (Kitengo A).

Wakati wa mchakato wa tathmini, AOC ilieleza CAO kuwa, ijapokuwa walikuwa na nia ya kushiriki kwenye Mradi kwenye Block 12A kati ya mwaka wa 2010 na mwaka wa 2017, hawakuendesha shughuli zozote na kuwa mwendesha shughuli katika kipindi hicho alikuwa Tullow kutokana na Mkataba wa Uendeshaji wa Pamoja uliofanywa na Tullow na AOC katika mwaka wa 2011. AOC walithibitisha kuwa walikuwa wameondoka kwenye Block 12A mwaka wa 2017, yaani, kabla ya CAO kupokea malalamishi.

Delonex walisema kuwa walimiliki hisa kwa Block 12A mwezi wa Septemba mwaka wa 2015 kwa mara ya kwanza na waliruhusiwa kuendesha shughuli na Tullow Januari mwaka wa 2018. Waliongezea kuwa hakuna uchimbaji wa wa kupelekea uzalishaji wa mafuta au gesi ulikuwa umewahi kuendeshwa na Delonex wakati wa shughuli zake.

³ Sera ya CAO inapatikana: <https://documents1.worldbank.org/curated/en/889191625065397617/pdf/IFC-MIGA-Independent-Accountability-Mechanism-CAO-Policy.pdf>.

⁴ Hivi ndivyo viwango vilivyoripotiwa katika ufichuzi wa IFC. Wakati wa kuzingatia uwekezaji unaopendekezwa, IFC hufichua taarifa muhimu kuhusu mradi, athari kwa mazingira na kwa jamii, na za maendeleo zinayotarajiwa kutokana na uwekezaji kwenye tovuti yake. Tazama www.ifc.org/disclosure.

IFC ilisema kuwa ijapokuwa inafuatilia shughuli za Delonex, kampuni ya Tullow haikuwa mteja wa IFC. AOC haikuendesha Shughuli kwenye Block 12A chini ya ufadhili wa IFC, na msaada uliotelewa na IFC kwa AOC ulilikuwa wa kununua vifaa vya kufanyia kazi ya Africa Oil.

Malalamishi

Mwezi wa Agosti mwaka wa 2019, CAO ilipokea malalamishi kutoka kwa KVCO kwa niaba ya wanajamii 140 kutoka katika kaunti za Baringo, Elgeyo Marakwet na Pokot Magharibi. Mbali na KVCO, walalamishi pia walisaidiwa na JCAP, shirika linaloshughulikia masuala ya kisheria lililo na makao yake makuu nchini Kanada. Malalamishi hayo yalilalamikia kutokuwa na taarifa kuhusiana na mradi na kutoshauriana na washikadau kuhusiana na shughuli zinazohusiana na mafuta na gesi katika Block 12A; kushindwa kushughulikia madhara makuu ya mradi; mazingira mabaya ya kufanyia kazi; unyanyasaji wa kijinsia; na athari kwa ardhi,⁵ kwa maji, kwa kipato kwa jumla na kwa mazingira; uvunjaji wa kanuni za Mfumo wa Uendelevu wa IFC. Kwenye malalamishi yao, na wakati wa tathmini na wa mchakato wa utatuzi wa mzozo, walalamishi pia walidai kuwa baadhi ya wanajamii wenzao walilikuwa wametishiwa na kupokea vitisho kutokana na malalamishi waliyotoa kuhusiana na Block 12A.

Tathmini ya CAO

Katika mwezi wa Septemba mwaka wa 2019, CAO ilibaini kuwa malalamishi yalilikidhi vigezo vyote vitatu vya utaratibu uliowekwa kuwezesha malalamishi kukubalika na ikaanza kufanya tathmini ya malalamishi. Nia ya tathmini ya CAO ni kuweka bayana mambo na masuala yaliyoibuliwa katika maalalamishi; kukusanya taarifa kuhusiana na maoni ya washikadau mbalimbali; na kubaini iwapo wahusika wangependa mchakato wa utatuzi wa mzozo, au iwapo wangependa malalamishi yashughulikiwe na kitengo cha Ridhaa cha CAO.

Katika mwezi wa Januari mwaka wa 2020, CAO ilifanya ziara nchini Kenya ili kuelewa vyema hali ilivyo na kujadili jinsi ya kushughulikia malalamishi na pande husika. CAO ilikutana na KVCO pamoja ya baadhi ya wanajamii (ambao baadhi yao walichaguliwa baadaye kama wawakilishi katika mchakato wa DR) kutoka katika maeneo ya Kerio Valley, Eldoret na Marakwet; wawakilishi wa AOC, Delonex, pamoja na wajumbe wa Bunge la Kaunti ya Baringo (MCA).

Wakati wa tathmini ya CAO, Delonex na Walalamishi waliamua kushughulikia masuala yaliyoibuliwa kupitia kitengo cha CAO cha Kutatua Mizozo. AOC ilidinda kushiriki katika mchakato huo. Mchakato huu wa tathmini ulichukua muda mrefu zaidi ya siku 120 za kawaida za kufanya kazi kama ilivyohitajika kipindi hicho kwa kuzingatia Miongozo ya Utendakazi wa CAO. Muda zaidi ulihitajika ili kukabiliana na masharti yaliyowekwa makali ya janga la korona (COVID-19) yalipozidi, na kutafuta Tullow, punde tu ilipobainika walikuwa washikadau muhimu.⁶ Tullow walitoa mtazamo wao kuhusu malalamishi kwa CAO na kuomba mtazamo

⁵ Baadhi ya Walalamishi walieleza kuwa utafiti wa kijiolojia ulisababisha mmomonyoko wa udongo na kuwa mashamba yao hayakuborehwa ipasavyo baada ya kukamilika kwa uauzi wa kijiolojia. Baadhi yao walidai kuwa hawakufidiwa ipasavyo kutokana na madhara yaliyosababishwa kwa ardhi, nyumba, na/au nyua kutokana na shughuli za uauzi wa kijiolojia.

wao kujumuishwa kwenye ripoti ya tathmini. Tullow pia ilionyesha kuwa kulikuwa na uwezekano wa wao kushiriki katika mazungumzo yaliyoongozwa na CAO kati ya walamishi na Delonex. Katika mwezi wa Oktoba mwaka wa 2020, CAO ilichapisha ripoti yake ya tathmini, inayotoa muhtasari wa mtazamo wa kila upande na matokeo ya tathmini.⁷

Mchakato wa Utatuzi wa Mzozo

Kujiandaa kwa majadiliano na kujengewa uwezo

CAO iliandaa mtandaoni vikao vya kujengea Delonex na Tullow uwezo mwezi wa Desemba mwaka wa 2020 na vikao na walalamishi katika mwezi wa Machi mwaka wa 2021. Kati ya Novemba mwaka wa 2020 na Januari mwaka wa 2021, KVCO ilisema kuwa waliandaa mikutano mingi katika jamii ili kukubaliana kuhusu wawakilishi mwafaka wa jamii watakaoshiriki katika mchakato wa utatuzi wa mzozo. Kutokana na mikutano hiyo, jamii ilichagua wawakilishi 16 kushiriki katika mchakato kwa niaba yao (wakijumuisha wanaume 11 na wanawake 5).⁸ Mwezi wa Februari mwaka wa 2021, CAO na walalamishi walishirikiana kutafuta mahali mwafaka pa kuendeshea vikao vya mtandaoni. Hoteli iliyo na mtandao wa intaneti na vifaa vya mikutano ilipatikana mjini Eldoret. Walalamishi walisafiri hadi huko na kuungana na CAO mtandaoni.

Vikao vyote vya kujengea uwezo vilijumuisha mafunzo kuhusu utatuzi wa mizozo, mawasiliano, na mchakato wa CAO.

Mchakato wa mazungumzo

CAO iliitisha mkutano wa kwanza wa pamoja mtandaoni mwezi wa Mei mwaka wa 2021 uliohudhuriwa na wawakilishi wa Delonex na Tullow, pamoja na walalamishi, waliowakilishwa na wanachama wa KVCO na wawakilishi waliochaguliwa kutoka kwa wanajamii.

Kabla ya kikao cha pamoja, CAO ilifanya mikutano kandokando na kila upande ili kutathmini misimamo na matamano yao na kuwatayarisha kwa kikao cha pamoja. Wakati wa vikao vya kandokando na CAO, Delonex ilisisitiza kuwa ilikuwa zaidi ya miaka miwili tangu walipokomesha shughuli zao nyanjani na kudai kuwa hakukuwa na dalili au taarifa kutoka kwa jamii kuhusu mzozo wowote uliokuwepo uliohitaji kushughulikiwa.

Wakati wa mkutano wa pamoja wa kwanza, majadiliano yalijikita kwa matarajio ya wahusika kwa mchakato na mambo yanayoweza kujumuisha kwa kanuni za kuongoza mazungumzo.⁹

⁶Tullow ndio ilikuwa inaendesha kwenye Block 12A kabla ya Delonex kuchukua awamu na masuala kadhaa ya malalamishi kuhusiana na wakati ambapo Tullow ilikuwa inaendesha shughuli. Kwa hivyo, kwa mapendekezo ya wahusika, CAO iliwasiliana na Tullow wakati wa tathmini ili kuelewa mtazamo wao kuhusu masuala katika malalamikshi.

⁷ Ripoti ya tathmini ya Oktoba mwaka wa 2020 inaweza kupatikana: https://www.cao-ombudsman.org/sites/default/files/downloads/CAOAssessmentReportDelonex_AfricaOil_01.pdf.

⁸ 8 kati ya wawakilishi hawa pia walikuwa wanachama wa KVCO. Wawakilishi mwanzoni mwa mchakato huo walikuwa kutoka kaunti za Baringo, Elgeyo Marakwet na Pokot. Wakati wa mchakato huo, wawakilishi wengine walibadilika.

⁹Kama sehemu ya mazungumzo kwa kuhusu mambo ya kujuisha katika kanuni za kuongoza mazungumzo, wahusika walijadili kuhusu maoni yao kuhusu jinsi ya kuzingatia kanuni ya usiri wakati wa mchakato, majumu yatakayotekezwa na wa tu waliopendekezwa kuhudumu kama washauri na waangalizi wakati wa mchakato na jinsi ya kushughulikia vitisho na kulipiza kisasi.

Wahusika pia walijadili kuhusu upeo wa mazungumzo, yaani, masuala makuu ambayo wangeyajadili katika mchakato.

Walalamishi walielezea matarajio yao kwamba majadiliano yangeweza kusaidia kukuza mahusiano ya kuaminiana kati yao, Delonex na Tullow na kutoa mfumo wa ushirikiano kati yao na Delonex baadaye, kampuni iliyochaguliwa kuendesha shughuli kuendelea mbele. Walielezea kuwa wangependelea kuwe na kushiriki kwa taarifa kuhusiana na shughuli za baadaye za Delonex katika Block 12A. Walalamishi pia walionyesha nia ya kujadili malalamishi yao ya awali na kutafuta njia za kuyashughulikia kwa ushirikiano na Delonex na Tullow, pindi tu wahusika watakapokubaliana kuhusu mambo ya kujumuisha katika kanuni za kuongoza mchakato.

Kwa upande wao, Delonex ilisisitiza kuwa hatua ya kwanza ni sharti walalamishi washiriki maelezo zaidi kuhusu malalamishi ili kuwezesha kuwa na uwezekano wa kuyashughulikia vyema. Delonex ilisema kuwa watu 140 waliokuwa na malalamishi ya awali ilikuwa idadi kubwa sana na kwamba baadhi ya malalamishi haya yalikuwa na uzito mkubwa na kushangaa kwa nini hayakutolewa kwa Delonex wakati ilipokuwa ikiendesha shughuli zake. Delonex ilisema kuwa ilikuwa imejumuisha jamii kupitia njia nyingi, rasmi na zisizo rasmi katika shughuli zake zote kwa kutumia kikosi kilicho na tajriba ya kiwango cha juu cha ushirikishaji wa washikadau ambacho kilikuwa kinajulikana sana katika jamii na kilipatikana kila mara wakati wote wa operesheni zake. Maoni ya Delonex yalikuwa kwamba walifurahia uhusiano mzuri wenye manufaa kwa jamii zote zilizoathiriwa. Waliongeza kuwa wangependa kuelewa vyema kutoka kwa walalamishi ikiwa malalamishi yaliyotajwa yalitokea wakati wa shughuli za hivi majuzi za Delonex.

Wahusika walikubaliana wakati wa mkutano huo kwamba suala la kwanza la msingi kujadiliwa katika mazungumzo ni malalamishi ya awali ambayo hayakutatuliwa.

Baada ya kikao cha pamoja, CAO iliunda rasimu ya kanuni za kuongoza mchakato kwa kuzingatia mambo yaliokuwa yamejadiliwa wakati wa mkutano, ambayo ilisambazwa kwa wahusika ili kuipitia. Wahusika hawakukubaliana kuhusu mambo ya kujumuishwa kwenye kanuni za kuongoza mchakato, ikijumuisha vipengele kuhusiana na kupashana habari pamoja na upeo wa mazungumzo. Wakati huu, kila upande ulitaka taarifa kutoka kwa ule upande mwingine. Hata hivyo hakuna upande uliotoa taarifa zilizohitajika. Kila upande ulilalamika kuhusu ule upande mwingine kwa kushindwa kutoa taarifa zilizohitajika, ambazo kila upande ulihisi kuwa zilikuwa muhimu kwa mchakato kuendelea mbele.

Ili kujaribu kupunguza kutofautiana kuhusu kanuni za kuongoza mchakato,¹⁰ CAO ilifanya diplomasia ya kiguu na njia (yaani, mikutano kandokando na kupitia barua pepe kati ya CAO

¹⁰Wahusika walishindwa kukubaliana kuhusu iwapo kanuni za kuongoza kikao zilikuwa muhimu na kipi kijumuishwe katika kanuni hizo.

na kila upande) kati ya Mei mwaka wa 2021 na Mei mwaka wa 2022. Hata hivyo kuna vipengele ambayo wahuwika waliendelea kutofautiana kuvihusu. Hatimaye walikubaliana kutia sahihi makubaliano ya usiri ili kuendelea kusonga mbele na mchakato na kushiriki katika mkutano wa pili wa pamoja.

Awali Tullow ilikuwa mwangalizi wa mazungumzo kuhusu kanuni za kuongoza mchakato. Hata hivyo, katika mwezi wa Novemba mwaka wa 2021, waliamua kujiondoa kwenye mchakato huo. Walieleza kuwa hawakuwa wakiendesha shughuli tena au kuwa washirika katika Block 12A na hawakuwahi kuwa wateja wa IFC wakati wa mradi huu, na kwamba manufaa ya wao kushiriki katika mchakato wa CAO wa utatuzi wa mzozo yalikuwa finyu. Waliongeza kuwa waliendelea kuunga mkono mchakato huo, ingawa sio kama mshiriki hai.

Katika mwezi wa Mei mwaka wa 2022, na kwa wito kutoka kwa Walalamishi, IFC ilifanya kikao cha kupashana habari kuhusu Viwango vya Utendakazi vya IFC kuhusiana na kushirikisha washikadau na mfumo wa kutatua mizozo.

Key Elements of a Grievance Mechanism for Affected Communities

- The Client is required to establish a grievance mechanism to receive and facilitate resolution of Affected Communities' concerns and grievances about the company's environmental and social performance.

Key elements:

- resolve concerns promptly
- Understandable and transparent
- Accessible and culturally appropriate

The mechanism should not impede access to judicial or administrative remedies

Process Flow:

- Report
- Receive and register
- Assess and address
- Track and document
- Adjust programs

Dondoo la wasilisho la powerpoint la IFC wakati wa kubadilishana taarifa mtandaoni kati ya IFC na walalamishi, Mei 2022

Mkutano wa pili mtandaoni ulifanyika mwezi wa Juni mwaka wa 2022. Wakati wa mkutano huu, Delonex ilieleza kwamba walikuwa wameondoka kwenye Block 12A (Februari mwaka wa 2022) na wala hawakuwa tena na leseni ya kuendelea kuendesha shughuli kwenye Block 12A. Delonex ilisisitiza kwamba ijapokuwa walikuwa wameondoka kwenye Block 12A, bado walikuwa tayari kujadili suala la malalamishi ya awali. Waliendelea kuisitiza ombi lao la kupokea taarifa kuhusu malalamishi ya awali, mambo kuyahusu, wakati yalipotokea, eneo na upeo, ili waweze kuyazingatia kwa undani.

Katika majadiliano yaliyofuata, walalamishi walieleza kuhusu kusikitishwa kwao kuhusu kujiondoa kwa Delonex katika Block 12A, hali iliyowafanya walalamishi kuhisi ilipelekea kuhitimika kwa uwezekano wa majadiliano kuhusu hatima ya Block hiyo na Delonex. Pia, walieleza kuwa hawakufahamu kwamba kulikuwa na mfumo wa kutatua mzozo wakati Delonex

ilipokuwa inaendesha shughuli zake kwenye Block 12A na kwamba hawakuwa wamewahi kupokea stakabadhi zozote kuhusu mfumo huo licha ya kuziomba wakati wa mchakato wa DR. Walipendekeza kujadiliana na kukubaliana na Delonex kuhusu mchakato wa viwango vya utendakazi vya IFC vya kushughulikia mizozo (GRM) ili kushughulikia malalamishi yao kabla ya kutoa maelezo zaidi kuliko ilivyotajwa kwenye malalamishi yao ya awali kabla ya kutoa maelezo zaidi kuhusu malalamishi hayo.

Delonex ilieleza kuwa ilikuwa na mfumo wa kutatua mzozo unaendena na vigezo vya IFC kipindi chote walipokuwa wanaendesha shughuli zao nchini Kenya, ambao walizungumza kuuhusu wakati wa mikutano na wanajamii, na ulitumiwa mno na jamii kutoa malalamishi yao wakati walipokuwa wanaendesha shughuli zao. Delonex walionekana kusikitishwa kuwa licha ya walalamishi kukubali ajenda kuu itakuwa “malalamishi ya awali” na Delonex walikuwa wameshatia sahihi makubaliano ya usiri, walalamishi hawakuwa tayari kutoa maelezo kuhusu malalamishi ya awali.

Kwa upande wao, walalamishi walieleza kuwa walihitaji kuelewa na kukubaliana juu ya utaratibu utakaofuatwa kushughulikia malalamishi yao kabla ya wao kuwa tayari kutoa maelezo zaidi kuhusu malalamishi hayo, hivyo basi wakatoa wito wa kujadili GRM.

Kikao kilihitimishwa kwa wahusika kukubaliana kubadilishana stakabadhi na habari na kukutana tena baada ya kubadilishana stakabadhi.

Uamuzi wa walalamishi kuhitimishaa mchakato wa Utatuzi wa Mzozo

Mda mfupi baada ya mkutano wa pili wa pamoja, walalamishi walitoa wito kwa CAO kuhitimisha mchakato wa utatuzi wa mzozo. Walieleza kuwa walihisi Delonex ilipaswa kufichua kujiondoa kwake kutoka kwa Bloku mapema mwanzoni mwa mchakato wa mazungumzo. Walieleza wasiwasi yao kuwa mchakato huo uliegemea upande mmoja tu, na kuwa walihisi kuwa Delonex ikikataa kushiriki stakabadhi nao huku wakiwashinikiza walalamishi kutoa maelezo ya kina kuhusu malalamishi yao ya awali. Walisikitishwa na kile walichokichukulia kama ukosefu wa uwazi kuhusu nia halisi ya kampuni kushughulikia malalamishi ya hapo awali, haswa ikizingatiwa imeondoka nchini Kenya.

Kwa upande wake, Delonex ilionyesha kufadhaika kutokana na walalamishi kutokuwa tayari kutoa taarifa kuhusu malalamishi ya awali licha ya kwamba walikuwa wamekubali kufanya hivyo katika mkutano wa awali. Ilisema kutopiga hatua kuhusiana na ombi hili lao kuu au kutokana la Delonex, angalau taarifa hizi zitolewe kwa CAO. Delonex iliongeza kuwa ulikuwa uamuzi wa Walalamishi kushiriki kwenye mchakato wa CAO wa kutatua mizozo kwa madhumuni ya kushughulikia malalamishi ya aina hii. Pia walisikitishwa kuwa vile vile, hakuna taarifa yoyote inayohusiana na madai ya suala la kupokea vitisho na kutishiwa wala unyanyasaji wa kijinsia ilitolewa kwao.

CHANGAMOTO MAMBO YA KUTAFAKARI NA MAFUNZO YALIYOPOKELEWA

Kesi hii ilikumbwa na changamoto kadhaa, mambo mengi ya kutafakariwa na fursa za kutoa mafunzo ikijumuisha yafuatayo:

Mapungufu ya utatuzi wa mzozo mtandaoni pale watu wanapoaminiana kwa kiwango kidogo

Kujadiliana na kuelewana wakati ambapo viwango vya kuaminiana viko chini (au hushuka mara kwa mara) ni changamoto kubwa sana mtandaoni. Ingawa CAO ilijitihidi kuwezesha makubaliano kuhusu rasimu ya kanuni za kuongoza mchakato kupitia majadiliano ya kandokando na kupitia barua pepe na kampuni na jamii na hatua kadhaa kupigwa, kuendesha mchakato mtandaoni kulikumbwa na changamoto na wakati mwingine hakungetegemewa. Ilikuwa vigumu kupunguza utata kuhusiana vifungu mahususi, kama vile upeo wa majadiliano na wajibu wa kubadilishana taarifa. Pia, wakati wote wa mchakato, kutoaminiana kuliendelea kuwepo kwa kiwango cha juu na kila upande kuuliza mara kwa mara iwapo ule upande mwingine ulikuwa na nia njema. Fursa za kujumuika wakati wa upatanisho kupitia vikao vya ana kwa ana huenda ingesaidia kuziba mapengo yanayohusiana na hofu na mashaka na pia kuhusu vifungu mahususi vyenye utata kama vile upeo wa mazungumzo na umuhimu wa kuaminiana kuwa na matokeo ya upatanisho yanayokubalika kwa pande zote.

Kanuni za kuongoza mchakato: baraka au laana?

Katika mazoea ya CAO, kuweka chini baadhi ya kanuni za kuongoza mchakato wa DR kwanza ni sehemu muhimu ya kuwezesha kuaminiana na kuelewana. Ingawa si michakato yote ya utatuzi wa mizozo huhitaji kanuni za kuongoza mchakato kabla ya kuanza, inaweza kusaidia wahusika kukubaliana kuhusu kanuni zitakazowaongoza katika mchakato mzima na ambazo mpatanishi anaweza kuzitumia kuhakikisha wanawajibika.¹¹ Mwanzoni mwa mchakato huu, kama sehemu ya kujengea uwezo, CAO ilitoa muhtasari wa hali ya kawaida ya mchakato wa kutatua mizozo, ikiwa ni pamoja na uundaji wa kanuni za kuongoza mchakato.

Katika kesi hii, kikosi cha CAO kilipata changamoto kwa jumla kutokana ma maslahi ya wahusika na uvumilivu wao wakati wa maandalizi ya awali na majadiliano kuhusu masuala ya utaratibu kukinzana. Ijapokuwa upande mmoja ulikuwa na nia ya kuweka kanuni imara na za kina za kuongoza mchakato ili kuweka mazoea bora, upande ule mwingine uliomba kuanza kwa majadiliano kuhusu masuala muhimu haraka iwezekanavyo, licha ya kutokuwa na makubaliano kuhusu usiri ambayo yalifikiwa baadaye. Majaribio ya mpatanishi kutaka wahusika kulegeza misimamo yao hazikuzingatiwa kila mara na wahusika na hii ilisababisha kwa pande zote mbili kufadhaika. Upande mmoja ulihisi kuwa mchakato huo ulikuwa unaharakishwa na kwamba matarajio yao ya kuwa na kanuni za kuongoza mchakato yalipuuzwa, huku upande ule mwingine ukiendelea kueleza kuwa haukuelewa kwa nini mwenzao hakuwa tayari kutoa maelezo kuhusu masuala muhimu.

Mapungufu ya mikutano ya kandokando na wahusika wakati wa upatanisho

Kati ya mwezi wa Mei mwaka wa 2021 na mwezi wa Mei mwaka wa 2022, wahusika hawazungumza moja kwa moja, isipokuwa kupitia CAO. Hali hii ilipelekea kutoelewana, na mtazamo wa pande zote mbili kuchukulia kwamba CAO ilikuwa inahimiza upande mmoja kulegeza msimamo, na wala siyo hivyo kwa upande ule mwingine. Zaidi ya hayo, CAO inawajibika kudumisha usiri wa taarifa inazopokea kutoka kwa mhusika, isipokuwa kama

¹¹ Tazama Mambo ya Kutafakari Kuhusu kutoka kwa Kazi ya CAO DR Reflections from Practice “Kuanza”, 2018: <https://www.cao-ombudsman.org/resources/reflections-practice-series-1-getting-started-dispute-resolution>

mhusika huyo atatoa idhini ya kuzifichua. Mikutano ya kandokando na wahusika pamoja na wajibu kama huu wa kudumisha usiri inaweza kudhuru pande zote. Ingawa ni muhimu kwa wahusika na kuendeleza mchakato, katika hali hii, kuna uwezekana ilipelekea kutoaminiana kati ya wahusika na kati yao na CAO. Hii inawezekana kwa sababu, kutokana na hali ya mikutano ya kandokando, wahusika hawakuweza kufahamu upeo wa kazi iliofanywa na kikosi cha wapatanishi kwa kila upande ili kuwezesha kufikia muafaka.

HITIMISHO NA HATUA ZINAZOFUATA

Licha ya juhudi za pande zote kujaribu kutatua masuala yaliyoibuliwa kwenye malalamishi, wahusika walishindwa kuafikiana. Kwa hivyo, kesi hiyo itahamishiwa kwa Kitengo cha Ridhaa cha CAO kwa wito kutoka kwa Walalamishi na kwa kuzingatia Sera ya CAO. CAO itafanya tathmini ya ridhaa kubaini kama uchunguzi wa utendakazi wa kimazingira na kijamii wa IFC unastahili kufanywa kuhusiana na masuala yaliyoibuliwa kwenye malalamishi, au iwapo kesi hiyo itafungwa.

Stakabadhi zote zinazohusiana na kesi hii zinapatikana kwenye tovuti ya CAO kupitia www.cao-ombudsman.org.

Pitia Kiambatisho A ili kupata taarifa zaidi kuhusu mchakato wa CAO.

KIAMBATISHO A. UTARATIBU UNAOFUATWA NA CAO KUSHUGHULIKIA MALALAMISHI

Punde baada ya CAO kutangaza kuwa malalamishi yanakubalika, tathmini ya kwanza hufanywa na wataalamu wa CAO wa kutatua mizozo. Nia ya tathmini ya CAO ni: (1) kubainisha masuala na malalamishi yaliyotolewa na Malalamishi/Walalamishi; (2) kutafuta taaarifa kuhusu jinsi washikadau wengine wanavyoonelea hali hiyo; na (3) kuwasaidia washikadau kuelewa njia wanazoweza kutumia kutatua mzozo na kubainisha iwapo wangependa kushirikiana kutafuta suluhu kupitia Kitengo cha Kutatua Mizozo cha CAO, au iwapo kesi hiyo inapaswa kushughulikiwa upya na Kitengo cha Ridhaa cha CAO.

Kwa kuzingatia Sera ya CAO ya Mfumo wa Uwajibikaji Unaojitegemea wa IFC/MIGA,¹² hatua zifuatazo hufuatwa ili kushughulikia malalamishi yaliopokelewa:

Hatua ya Kwanza: **Kukubali** kuwa malalamishi yamepokelewa.

Hatua ya Pili: **Kukubalika**: Kubainisha iwapo malalamishi yanakubalika kufanyiwa tathmini na CAO (hii hufanyika kwa siku za kufanya kazi zisizozidi 15).

Hatua ya Tatu: **Tathmini**: Kutathmini maswala na kuwasaidia washikadau kuyaelewa na kubainisha iwapo wangependa kushirikiana kupata suluhisho chini ya usaidizi wa kitengo cha CAO cha Kutatua Mizozo, au iwapo kesi hiyo inapaswa kushughulikiwa na kitengo cha Ridhaa cha CAO ili kuchunguza iwapo utaratibu wote wa kimazingira na kijamii unaotolewa na IFC/MIGA umefuatwa kikamilifu. Mda wa kutathmini unaweza chukua kwa ujumla siku za kufanya kazi 90, kukiwa na uwezekano wa kuongeza tu siku 30 zaidi za kufanya kazi, iwapo mda utazidi mda wa kufanya kazi wa siku 90: (1) Wahusika wanathibitisha kwamba utatuzi wa malalamishi unawezekana au (2) Upande wowote unaonyesha nia ya kutatua mzozo, na kuna uwezekano kwamba Upande huo mwingine utakubali.

Hatua ya Nne: **Kuwezesha usuluhishaji**: Iwapo wahusika watakubali kushirikiana kutatua mzozo, Kitengo cha CAO cha Kutatua Mizozo kitahusika. Mchakato wa utatuzi wa mzozo huzingatia au kufuata Mkataba wa Maafikiano na/au kutumia sheria zinazowekwa chini na kukubaliwa na Wahusika wote. Inawezahusisha kusaidiwa/upatanisho, kushirikiana kutafuta ukweli, au njia yoyote itakayokubaliwa inayoweza kuleta suluhisho au kusaidia kufikia malengo yaliyowekwa kwa pamoja au malengo mwafaka. Lengo kuu la kutumia njia hizi kutatua mzozo ni kushughulikia masuala yanayojitokeza kwenye malalamishi, na masuala mengine yoyote muhimu yanayohusiana na malalamishi yaliyojitokeza wakati wa kutathmini mzozo au wakati wa mchakato wa utatuzi wa mzozo kwa njia inayokubalika kwa pande zinazohusika.¹³

¹² Kwa maelezo zaidi kazi na wajibu wa CAO, tafadhali rejelea Sera ya CAO ya Mfumo wa Uwajibikaji Unaojitegemea wa IFC/MIGA: <https://documents1.worldbank.org/curated/en/889191625065397617/pdf/IFC-MIGA-Independent-Accountability-Mechanism-CAO-Policy.pdf>

¹³ Pale ambapo washikadau watahindwa kutatua matatizo kwa ushiriakiano kwa mda uliowekwa, Kitengo cha CAO cha Kutatua Mizozo kitaanza kwa kujaribu kusaidia washikadau kukabiliana na changamoto. Iwapo haitawezekana, kikosi cha Kutatua Mizozo kitawaeleza washikadau, wakiwemo wafanyikazi wa IFC/MIGA, Rais

AU

Kutathmini kwa Ridhaa/Uchunguzi: Iwapo wahusika watachagua uchunguzi kufanywa, malalamishi yatahamishiwa kwa Kitengo cha Ridhaa cha CAO. Malalamishi pia huamishiwa kwa Kitengo cha Ridhaa cha CAO iwapo mchakato wa utatuzi wa mzozo utapelekea makubaliano kwa kiwango fulani au kutokuwa na makubaliano kabisa. Angalau Malalamishi mmoja anapaswa kutoa ruhusa wazi ya kuyahamisha, au iwapo CAO inafahamu kuhusu tuhuma za Vitisho na Kulipiza Kisasi. Kitengo cha Ridhaa cha CAO kitafanya uchunguzi kubaini iwapo sera zote za kimazingira na kijamii zilizowekwa na IFC/MIGA zimezingatiwa kutathmini madhara yanayoweza kutokea na kupendekeza hatua mwafaka zinazohitaji kuchukuliwa kwa kuzingatia mchakato wa hatua tatu. Kwanza, tathmini ya kitengo cha ridhaa huamua ikiwa uchunguzi zaidi unahitajika. Tathmini inaweza kuchukua hadi siku 45 za kufanya kazi, na ina uwezekano wa kuongeza siku 20 za kufanya kazi katika hali za kipekee. Pili, uchunguzi ukihhitajika, tathmini inafuatwa na uchunguzi wa kina wa ridhaa kwa kuzingatia utendakazi wa IFC/MIGA. Ripoti ya uchunguzi itatolewa kwa umma, pamoja na majibu ya IFC/MIGA pamoja na mpango wa utekelezaji wa kushughulikia matokeo ya kutoridhia na madhara husika. Tatu, katika hali ambapo kutoridhia na madhara vitabainika, CAO itafuatilia utekelezaji mzuri wa mpango kazi.

Hatua ya Tano: **Ufuatiliaji**

Hatua ya Sita: **Hitimisho/Kufungwa kwa Kesi**

na bodi ya Benki ya Dunia, na umma kuwa, Kitengo cha CAO cha Utatuzi wa Mizozo kimefunga malalamishi na kuyahamishia kwa Kitengo cha Ridhaa cha CAO ili kutathminiwa.